Sylvance

KITANGULIZI MWIGO 2022

MWONGOZO

KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

1. **Wewe ni katibu wa Tume ya kitaifa iliyoteguliwa na Waziri wa Usafiri kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani. Andika ripoti ya uchunguzi wenu.**

**SURA**

Hii ni insha ya ripoti kwa hivyo inachukuwa muundo wa ripoti rasmi.

**Kichwa**

Kirejelee ripoti, tume iliyoteuliwa na waziri wa usafiri kuhusu vyanzo vya ajali barabarani.

Bila kichwa aondolewe alama 2; za anwani

**Utangulizi**

Mtahiniwa atangulize kwa kurejelea tume ya kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani. Kipindi cha utafiti, mteuzi wa tume – Waziri wa Usafiri.

Bila utangulizi, ondoa 4S

**Hadidu za rejea** – ila sio lazima

**Mbinu za utafiti**

Mtahiniwa aeleze kwa kina kati ya mbinu zifuatazo walizozitumia kukusanya data.

- Mahojiano
- Hojaji
- Utafiti wa maktabani
- Uchunzaji
- Kushiriki

Bila kurejelea mbinu za kukusanya data, ondoa 4S

**Matokeo**

Baadhi ya matokeo ni kama yafuatavyo;

- Njia/ barabara mbovu
- Magari mabovu barabarani
- Madereva wasiohitimu vizuri
- Kuendesha magari kwa kasi
- Kubeba abiria na mizigo kupita kiasi
- Polisi fisadi
- Watumizi wabarabara kutokuwa waangalifu/makini
- Ulevi
- Kutodhibiti usukani vizuri
- Uchovu na kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika
- Matimizi mabaya ya dawa za matibabu
- Matumizi ya dawa za kulevya
- Mzongo wa mawazo
- Usumbufu kutoka kwa abiria

**Tanbihi:** mtahiniwa arejelee hoja saba na kueleza vizuri kwa kutumia mada ndogo ndogo/ aya.

**Mapendekezo**

- Wavunja sheria kuchukuliwa hatua za kisheria
- Kuondoa plisi fisadi barabarani
- Kukarabati barabara vizuri
- Ukaguzi wa mara kwa mara wa magari
- Mafunzo mazuri ya mara kwa mara ya madereva
- Magari kuwekewa vidhibiti mwendo
- Matumizi ya mikanda ya usalama
- Vifaa vya kutambua madereva walevi
- Madereva kuwa waangalifu na makini.
- Watumizi wengine wa barabara kuwa makini na waangalifu
- Madereva walio na mzongo wa mawazo kutoruhusiwa kuendesha magari.

**Hitimisho**

Mtahiniwa atoe mhutasari au shukrani kwa mteuzi wa tume pamoja na walioshiriki katika utafiti.

Akikosa hitimisho; ondoa 4S

Bila sehemu za sura 4S

Kutafuta sasa.

**Ithibati**

Hii ndio sehemu ya mwisho

Mtahiniwa aonyeshe ripoti imeandikwa na nani.

Sahihi

Jina

Cheo- Katibu wa Tume ya uchunguzi wa vya vya ajali barabarani

Bila sehemu hii –ondoa alama 4S

2. **Jadili mikakati ambayo serekali imeweka kuimarisha sekta ya viwanda nchini.**

**Muundo**

Hii ni insha ya kueleza au kufafanua

Kichwa

Kizizidi maneno sita na kilenge mada

Bila kichwa ondoa alama 2A

**Utangulizi**

Sio lazima lakini ni upekee wa mtahiniwa.

**Mwili**

- Baadhi ya hoja ni kama zifuatazo;
- Kuimarisha miundomsingi ya barabara
- Kuimarisha miundomsingi ya nishati/stima/kawi
- Kuimarisha miundomsingi ya reli
- Kuimarisha miundomsingi ya viwanja vya ndege
- Kuimarisha miundomsingi ya bandari
- Kuimarisha vyuo vya kiufundi ili kutoa wataalamu
- Kuimarisha sekta ya kilimo ili kutoa maligghafi hasa kwa viwanda vya kizaraa
- Serikali kutoa mikopo ya riba ya chini
- Serikali kutoa ruzuku kwa pembejeo na kwa wafanyibiashara ili kuhimiza uwekezaji wan je na ndani
- Utafiti kuhusiana na madini muhimu kama vile mafuta, dhahabu n.k
- Kutoza ushuru wa chini ili kuwavutia wekezaji wa nje na ndani
- Kupanua sekta ya kibinafsi

**Tanbihi:** mtahiniwa azingatie hoja saba kama maudhui

**Hitimisho**

Si lazima lakini ni upekee wa mtahiniwa

3. **Tunga kisa kinachoafiki matumizi ya methali hii:**

Mhini na mhiniwa njia yao moja.

**Muundo**

Hii ni insha ya methali.

Muundo uchukuwe sura ya methali

**Kichwa**

Kiwe methali yenyewe- Mhini na mhiniwa njia yao moja.

Akibadilisha muundo wa methali atuzwe bakishishi. BK-01

Insha bila kichwa aondolewe alama 4S

**Utangulizi**

Si lazima lakini anaweza kutoa maana ya methali

**Mwili**

Kisa kilenge sehemu mbili ya methali. Sehemu ya mhini na sehemu ya mhiniwa

Bila sehemu mbili, atakuwa amepungukiwa kimaudhui kwa hivyo atuzwe bakishihsi- BK01

Mhini – mtu anayefanyia mweziwe maovu

Mhiniwa – anayefanyiwa maovu

Njia yao ni moja – wote hupata hasara

CamScanner

**Hitimisho**

Sio lazima lazima anaweza kutoa funzo kama upekee wake.

4. **Niliamshwa na sauti ya dirisha likifunguliwa polepole. Nje kulivaa weusi wa kutisha ...**

Endeleza kisa hiki.

**Muundo**

Hii ni insha ya ubunifu

Mtahiniwa abuni kisa kimoja.

**Kichwa**

Kizizidi maneno sita

Bila kichwa ondoa alama ~~4S~~ 2A

**Utangulizi**

Utangulizi urejelee mdokezo bila kubadilisha chochote. Mwanafunzi akibadili atakuwa amejitungia swali. Atuzwe bakishishi – BK-01

**Mwili**

Kisa kilenge maana ya mdokezo;

Kisa kitendeke nyakati za usiku

Kiwe cha kutisha sito – BK 01.

Mhusika ajihusishe na kisa,hivyo atumie nafsi ya kwanza.

Kisa kitendeke baada ya mhusika kuamka

Bila mwelekeo huu, mtahini atakuwa amepotoka kimaudhui, hivyo atuzwe bakishishi- BK-01

**Hitimisho**

Irejelee mwisho wa kisa. Amepungukiwa Kimaudhui

~~Kisa kikikosa hitimisho ondoa alama 4S.~~

CS CamScanner